
Jarida la

# SIHA NA MAENDELEO

UTAWALA BORA

www.sihadc.go.tz | Mwezi Agosti 2025 | Toleo la 26 | Halmashauri ya Siha



Haliuzwi

# WAZIRI BASHUGWA AZINDUA KITUO CHA POLISI, AWAPA HEKO WANANCHI SIHA




*Waziri wa mambo ya ndani ya nchi Mhe. Innocent Bashungwa Agosti 06, 2025 akizindua kituo cha polisi Wilaya ya Siha cha daraja B kilichojengwa kwa ushirikiano wa wananchi wa wilaya ya Siha na Serikali kwa jumla ya shilingi Milioni 522.5.*

Waziri wa mambo ya ndani ya nchi Mhe. Innocent Bashungwa amewashukuru wananchi wa Wilaya ya Siha na wadau wa maendeleo kwa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa kituo kipya cha polisi Siha cha daraja B kwa kuchangia shilingi milioni 179.4.

Waziri Bashungwa ametoa shukrani hizo Agosti 06, 2025 wakati wa uzinduzi wa kituo cha kipya cha polisi Siha cha daraja B kilichojengwa kwa ushirikiano wa wananchi wa wilaya ya Siha na Serikali kwa jumla ya shilingi Milioni 522.5.

Amesema ushirikiano huo kati ya wananchi na jeshi la polisi ni kielelezo cha utekelezaji wa dhana ya polisi jamii na jambo ambalo serikali inajivunia.

Naye, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini IGP. Camillus Wambura amesema Serikali imekamilisha na inaendelea kujenga miradi mbalimbali ya majengo na ofisi za polisi nchi nzima ambapo jumla ya miradi ya ujenzi wa majengo ya jeshi la polisi 164 ikiwa ni majengo mapya na majengo yaliyofanyiwa ukarabati mkubwa kama ilivyo Wilaya ya Siha.

Amesema miradi ya ujenzi na ukarabati wamajengo uliokamilika ina thamani ya shilingi Bilioni 32.44 huku miradi inayoendelea kutekelezwa nchi nzima ina thamani ya shilingi Bilioni 42.65.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu amesema kujengwa kwa vituo vipya vya polisi Mkoa wa Kilimanjaro ni kuimarisha usalama wa watu na mali zao.



*Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Innocent Bashungwa Agosti 06, 2025 akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wa serikali na dini baada ya kuzindua kituo cha polisi Wilaya ya Siha cha daraja B.*





*Waziri wa mambo ya ndani ya nchi Mhe. Innocent Bashungwa akiotesha mti wa kumbukumbu baada ya kuzindua kituo cha polisi siha cha daraja B Agosti 06, 2025.*





*Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini IGP. Camillus Wambura akiotesha mti wa kumbukumbu baada ya kuzindua kituo cha polisi siha cha daraja B Agosti 06, 2025.*





*Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu akiotesha mti wa kumbukumbu baada ya kuzindua Kituo kipya cha Polisi Siha cha daraja B Agosti 06, 2025.*

# TUFUATE MISINGI YA UADILIFU NA UWAJIBIKAJI – DKT TIMBUKA



*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka akizungumza kwenye Mkutano wa uchaguzi wa viongozi wa bodi ya maji ya Lawate – Fuka uliofanyika Agosti 19, 2025 katika ukumbi wa RC – Sanya Juu.*

Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka amesihi viongozi wapya wa bodi ya maji ya Lawate – Fuka waliochaguliwa kufuata misingi ya uadilifu na uwajibikaji ili kutatua kero na malalamiko ya wananchi katika kata zote tisa zinazohudumiwa na bodi hiyo.

Mhe. Dkt Timbuka ametoa rai hiyo Agosti 19, 2025 kwenye Mkutano wa uchaguzi wa viongozi wa bodi ya maji ya Lawate – Fuka uliofanyika katika ukumbi wa RC – Sanya Juu ambapo amewahimiza kufanya kazi kama timu moja ili wananchi wanaohudimiwa na bodi hiyo wapate huduma ya maji.

Amewasihi viongozi wote kushirikiana na kuwa wafuatiliaji ili kubaini sababu zinazochangia kukatika kwa maji na kuwafahamisha wananchi.

Amewaelekeza viongozi wa bodi waliochaguliwa kushirikiana wa wakala wa maji safi na usafi wa mazingira Wilaya (RUWASA), wenyeviti wa vijiji na watendaji wa kata na vijiji kubaini na kuzishughulikia changamoto au kero zinazoibuliwa na wananchi kwa wakati.

Naye, Mwenyekiti mpya wa bodi ya maji ya Lawate - Fuka Ndg. Nicholas Kombe amewashukuru wajumbe wa bodi kwa kumchagua na kuwaomba waendeleze ushirikiano ili kuwatumikia wananchi wa Wilaya ya Siha.




*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka akiwa kwenye picha ya pamoja na kamati tendaji mpya ya bodi ya maji ya Lawate – Fuka baada ya Mkutano wa uchaguzi wa viongozi hao uliofanyika Agosti 19, 2025 katika ukumbi wa RC – Sanya Juu.*






*Wajumbe wa Mkutano wa bodi ya maji Lawate – Fuka wakiwa kwenye Mkutano wa uchaguzi wa viongozi wa bodi uliofanyika Agosti 19, 2025 katika ukumbi wa RC – Sanya Juu.*

# VOYOTA YATOA MAFUNZO YA MRADI WA AJIRA YANGU KWA VIJANA KUINUA KILIMO WILAYA YA SIHA




*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Bi. Hellen Mwambeta (katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mkuu wa Divisheni ya Kilimo Mifugo na Uvuvi Dkt. Barnabas Mbwambo (pili kulia) na Wadau wa Kilimo kutoka shirika la Voice of Youth Tanzania (VOYOTA) agosti 11, 2025 baada ya kufungua mafunzo ya mradi wa vijana wa Ajira yangu katika ukumbi wa makao makuu ya Halmashauri.*

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha Bi.Hellen Emmanuel Mwambeta afungua mafunzo ya Mradi wa Vijana unaojulikana kwa jina Ajira yangu unaofadhiliwa na Shirika lisilo la Kiserikali VOYOTA (Voice of Youth Tanzania) katika Ukumbi wa Halmashauri ya Siha tarehe 11 Agosti, 2025

"Napenda kuwashukuru VOYOTA Kwa kuichagua Wilaya ya Siha kuwa miongoni mwa Wilaya chache za mfano hapa Tanzania zinazonufaika na mradi huu wa miaka mitatu 2024 hadi 2027" alisema Hellen Mwambeta

Kabla ya ufunguzi Mkurugenzi wa Shirika la VOYOTA ndugu Vincent Uhega alimshukuru Bi.Hellen Mwambeta Mkurugenzi Mtendaji SIHA DC kwa Mapokezi yake mazuri na ushirikiano wa dhati walioupata katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha

Alieleza kuwa mradi huu ni wa miaka mitatu kuanzia 2024 Hadi 2027 na unalengo la kuwajengea uwezo Vijana katika kuimarisha uchumi kupitia sekta ya Kilimo cha Kisasa ambacho mkulima ananza kutafuta soko kabla hajaingia shambani













*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Bi. Hellen Mwambeta (katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mkuu wa Divisheni ya Kilimo Mifugo na Uvuvi Dkt. Barnabas Mbwambo (pili kulia) na Wadau wa Kilimo kutoka shirika la Voice of Youth Tanzania (VOYOTA) agosti 11, 2025 baada ya kufungua mafunzo ya mradi wa vijana wa Ajira yangu katika ukumbi wa makao makuu ya Halmashauri.*





*Washiriki wa mafunzo ya mradi wa vijana wa ajira yangu yaliyotolewa na shirika la Voice of Youth Tanzania (VOYOTA) agosti 11, 2025 katika ukumbi wa makao makuu ya Halmashauri.*

Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha 5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677 Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz

# KAMATI YA USALAMA SIHA YAKAGUA MIRADI YA MAENDELEO




*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka akiiongoza Kamati ya Usalama Wilaya kukagua ukamilishaji wa miradi ya ujenzi wa wodi ya upasuaji wanawake, wodi ya upasuaji wanaume, wodi ya magonjwa ya ndani wanawake, jengo la kuhifadhi maiti na njia za waenda kwa miguu (walk ways) katika Hospitali ya Wilaya ya Siha.*






*Muonekano wa miundombinu iliyokaguliwa na Kamati ya Usalama Wilaya ya Siha Agosti 20, 2025 katika Hopitali ya Wilaya ya Siha.*













*Muonekano wa miundombinu ya awamu ya pili ya mradi wa ujenzi wa shule ya wasichana Kilimanjaro iliyokaguliwa na Kamati ya Usalama Wilaya ya Siha Agosti 20, 2025 inayotekelezwa kwa shilingi Bilioni 1.45*

# BWALO LA WANAFUNZI SHULE YA MSINGI SIHA




*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka Agosti 20, 2025 akiiongoza kamati ya usalama kukagua mradi wa ujenzi wa bwalo la wanafunzi katika Shule ya Awali na Msingi Siha lililojengwa kwa shilingi milioni 50 kutoka Serikali Kuu*






*Muonekano wa mradi wa bwalo katika shule ya awali na Msingi Siha lililokaguliwa na Kamati ya Usalama Wilaya ya Siha Agosti 20, 2025.*





*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka Agosti 21, 2025 akiiongoza kamati ya usalama kukagua mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Lawate unaotekelezwa kwa shilingi milioni 681.54 kutoka Serikali kuu*









*Muonekano wa mradi wa kituo cha afya lawate unaotekelezwa katika kijiji cha Lawate, Kata ya KIrua kwa Shilingi milioni 681.54 uliokaguliwa na Kamati ya Usalama Wilaya ya Siha Agosti 21, 2025.*

# SIHA YAFANYA VEMA MAONESHO YA NANE NANE ARUSHA




*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christoopher Timbuka (kwanza kulia) akiwa katika kilele cha maadhimisho ya siku Nane Nane yaliyofanyika katika viwanja vya maonesho Njiro jijini Arusha Agosti 08, 2025*

Kamati ya maonesho ya 31 ya kilimo, mifugo na uvuvi (Nane Nane) kwa mwaka 2025 kanda ya kaskazini imeitunukia Halmashauri ya Wilaya ya Siha tuzo ya mshindi wa tatu mazao, Halmashauri katika kundi la wakulima na wafugaji ikiwa ni ishara ya kutambua kazi kubwa inayofanywa na wakulima na wafugaji Wilaya ya Siha kwa kulima kisasa na kuyaongeza thamani mazao ya kilimo

Tuzo hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu katika kilele cha maadhimisho ya nane nane Agosti 08, 2025 yaliyofanyika kwenye viwanja vya njiro jijini Arusha.

Pamoja na tuzo hiyo iliyotolewa kwa Halmashauri, mshindi wa jumla wa kilimo mifugo na uvuvi katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha ni Humphrey Herman Mosha huku mshindi wa tatu wa paredi ya mifugo, ng'ombe wa nyama akiwa Daud Ndapashi kutoka Halmashauri ya Siha.

Maonesho ya Nane Nane kwa mwaka 2025 yaliongozwa na kaulimbiu inayosema, "Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi"




*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Bi. Hellen Emmanuel Mwambeta akikagua banda la wajasiriamali wa Wilaya ya Siha wanaoongeza thamani mazao ya kilimo.*







*Shughuli mabalimbali za maoenesho ya nane nane zikiendelea katika banda la kilimo na mifugo katika viwanja vya Njiro, Jijini Arusha.*

## UCHAGUZI MKUU 2025




*Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Siha Ndg. Marco Masue amemteua Dkt. Godwin Oloyce Mollel kuwa Mgombea Ubunge Jimbo la Siha kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) Agosti 27, 2025.*

*Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Siha Ndg. Marco Masue amemteua Ndg. Ashukuriwe Goodluck Matemu kuwa Mgombea Ubunge Jimbo la Siha kupitia Chama cha ACT Wazalendo Agosti 27, 2025.*




*Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Siha Ndg. Marco Masue amemteua Ndg. Daudi Wilibrod Mtuyehabi kuwa Mgombea Ubunge Jimbo la Siha kupitia Chama cha Wananchi (CUF) Agosti 27, 2025.*




*Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Siha Ndg. Marco Masue amemteua Bi. Daniela Msila kuwa Mgombea Ubunge Jimbo la Siha kupitia Chama cha Makini Agosti 27, 2025.*




*Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Siha Ndg. Marco Masue amemteua Bi. Anna Thobiasi Kipembela kuwa Mgombea Ubunge Jimbo la Siha kupitia Chama cha National Reconstruction Alliance Agosti 27, 2025.*




*Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Siha Ndg. Marco Masue amemteua Ndg. Mdoe Yambazi Azaria kuwa Mgombea Ubunge Jimbo la Siha kupitia Chama cha Sauti ya Umma (SAU) Agosti 27, 2025.*




*Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Siha Ndg. Marco Masue akibandika fomu za uteuzi za wagombea Ubunge wa Jimbo la Siha Agosti 27, 2025*






*Fomu za uteuzi wa kugombea Ubunge Jimbo la Siha zikiwa zimebandikwa katika eneo la wazi baada ya kuteuliwa Agosti 27, 2025.*

## MICHEZO NA BURUDANI















## SHIMISEMITA 2025 - TANGA

# FURSA ZA UTALII WILAYA YA SIHA














***WATALII WA NDANI WAKIFURAHIA VIVUTIO VYA UTALII VILIVYOPO KATIKA WILAYA YA SIHA***



**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha**
**5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha**
**Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677**
**Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz**

**Tunapatikana**